

KWA NINI?



Mambo yote yanawezekana, Bwana naamini;
Bwana, naamini, Bwana, naamini,
Mambo yote yanawezekana, Bwana, naamini.

² Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

³ Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unaujua moyo wa mwanadamu. Na jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya wakati huu wa—wa ushirika wa kiroho na kuabudu pamoja na watu hawa wapendwa katika Uwepo wa Roho Mtakatifu.

⁴ Ee Mungu, tunaomba ya kwamba utalibariki kanisa hili dogo na makanisa yake yote madogo shirika kila mahali, shule. Wabariki watu Wako kila mahali, Baba. Jitwalie Mwenyewe utukufu, na useme nasi sasa, zaidi katika Neno. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁵ Mwaweza kuketi. Ndugu Williams, wote wawili Mkubwa na Mdogo, Ndugu Osborn, na ndugu na dada, naomba lisife kamwe, na liendeleo kuwa hai. Nina furaha sana asubuhi ya leo kujua, baada ya yote haya, yapata miaka kumi na minne, kurudi katika kanisa hili na kumwona Roho yule yule mtukufu akitenda kazi miongoni mwa watu. Ni lulu kubwa sana, Uwepo mkuu sana wa Mungu, ni adimu sana. Ninyi, nina hakika asubuhi ya leo, hamtambui jinsi mlivyofanikiwa. Ni raha sana kwa macho yangu kuangalia nyuso za watu na kuona utukufu wa Mungu ukiangaza.

⁶ Mimi na Ndugu Tommy tulikuwa tumeketi pale, hata tukiwaangalia wasichana wadogo na wavulana wadogo wakiingia katika ibada hiyo ya Bwana, kuwaona wanawake, wasichana wadogo, wa makamu, wazee, na wote, wameosha nyuso na ni safi, wanaume wakiongea kutoka mioyoni mwao. Ninyi... Nina hakika imetumika, mumelizoea tu, kwa sababu ni jambo la kila siku kwenu, bali kwangu mimi ni lulu.

⁷ Wakati mmoja kulikuwako na m—mzee mvuvi akitoka baharini na mtu akienda baharini kupumzika. Naye huyo mtu alikuwa amefanya kazi, alikuwa ni mwanasanaa, naye akasema alikuwa anaenda kupumzika, kwa hiyo akashuka baharini. Hakuwa amewahi kuiona hapo kabla, alikuwa amesoma habari zake, akaona picha zake, bali hakuwa amewahi kuiona hapo kabla. Basi akienda zake asubuhi hiyo, akishuka kwenda ufukoni mwa bahari, alikutana na mwanamaji aliyebobea au baharia mzee akitoka baharini, naye akasema, “Unaenda wapi, mtu wangu mwema?”

⁸ Akasema, “Loo, bwana, ninashuka kwenda kujipumzisha, ninashuka kwenda baharini.” Akasema, “Nina shauku sana ya

kusikia harufu ya chumvi kutoka kwenye mawimbi ya bahari yakirukaruka, na kuchezecheza ufukoni. Ninataka kusikia mlilo wa shakwe wa baharini anapopita.” Naye akajaribu kueleza jinsi alivyokuwa . . . kile alichokuwa anaenda kufanya.

⁹ Ndipo maskini huyo baharia akamwambia, kasema, “Sioni kitu cha kuvutia sana kwake, lakini nimekuwa humo kwa miaka arobaini. Sioni kitu cha kuvutia kwake.”

¹⁰ Nafikiri hiyo ndiyo shida. Mnaona? Kamwe hamtambui, mko tu moja kwa moja ndani yake wakati wote, mnaona, lakini kwangu mimi ni—ni shada kutoka Mbinguni, hiyo ni kusema, ni kitu halisi. Mnaona, unaweza kuzoea kitu chochote sana mpaka hakikuvutii, sana. Lakini inapofikia mahali ambapo ume—umesoma habari zake, umesikia habari zake, kisha uingie moja kwa moja ndani yake, kuna jambo tu ambalo hu—huninii . . . una—kwa namna fulani unapungukiwa na maneno ya kusema.

¹¹ Nilikuwa na yubile ndogo, sasa majuma machache yaliyopita kwenye kanisa la Ndugu Outlaw huko—huko Arizona. Kamwe si—sikuelewa. Nilikuwa . . . naenda . . . kazi yangu miongoni mwa watu, nami hujaribu kutembelea kila shirika, dhehebu, nikijaribu kufanya kazi vizuri niwezavyo, nikisimama katika pengo kwa ajili ya watu. Nilipoenda kule siku hiyo, na kuliangalia kundi hilo, na kusikia kwaya hiyo ikiimba kama asubuhi ya leo, na kuwaona hao vijana wanaume na wasichana wamesimama pale, katika ninii tu . . . nyuso zao zikimetameta, kuangalia nje na kumwona mzee ameketi pale, macho yao yakimetameta vivyo hivyo, nguvu za Mungu, nilishusha tu ukosi wangu, na kutupa koti langu, na . . . Kisha kuingia ndani yake tena asubuhi ya leo. Labda kama ningeninii . . . kupitia juma lingine sasa, inaonekana, pamoja nanyi. Kwa namna fulani kuna . . . Vizuri sana.

¹² Ndugu Williams, Mungu daima awe pamoja nawe na mwanao katika kazi hii kuu. Ndugu, hapa, wamishenari, na kadhalika, jinsi ninavyoathamini hili! Kamwe, kamwe msiliondokee, enyi marafiki, dumuni nalo, dumuni nalo, mnaona. Kamwe msiache roho hiyo ya ibada, na huo utakatifu safi ufe kamwe miongoni mwenu, idumisheni Nuru hiyo ikiwaka, kwa kuwa ndiyo tegemeo la Kanisa, hiyo ni kweli, ni Kristo katika Kanisa Lake.

¹³ Ningeweza tu kusimama na kuzungumza nanyi kwa muda mrefu, lakini nina mkutano mwingine unaokuja baada ya muda mfupi, nami, kwa kawaida kabla ya ibada hizo za uponyaji, ninapenda kukaa tu katika Uwepo wa Mungu kwa muda kidogo, na kufika kule, na kuomba, na kukesha, na kungojea mpaka nijue Uwepo Wake upo. Nao watakuwa na mstari wa maombi alasiri ya leo, naamini.

¹⁴ Si—siwezi kuahidi ni lini hasa, lakini nashangaa kama nikipitia . . . Ninayo anwani yenu hapa sasa, sikujua mlikuwa

wapi. Mimi hupitia barabara hii inayolipiwa ushuru mara nyingi nikienda magharibi. Kama ikitokea nipitie hapa kwenye usiku wa ibada, nitaingia iwapo mtaniambia tena namna hiyo. Hilo—hilo linafufua tu. . . Na—napenda hilo.

¹⁵ Sasa, kamwe nisingeweza kuimba. Siwezi kubeba sauti ikaniokoe, lakini mwajua, moja ya siku hizi ninyi nyote mtakapofika Nyumbani katika jumba lenu kubwa huko juu ya kilima, mwajua, na kuna kibanda kidogo, nafikiri, kwa ajili yangu, huko chini kabisa kwenye kona ya mwitu kule chini, kwa hiyo, asubuhi moja ukisimama nje barazani mwako, ukiangalia kando ya vilima na kuona nyota za asubuhi zikiimba pamoja, huko chini kabisa mwituni usikie wimbo ukija, “Neema ya Ajabu! jinsi hiyo sauti ilivyo tamu,” useme, “Vema, Mungu asifiwe, maskini Ndugu Branham alifaulu. Huyu hapo, yuko kule chini akiimba tu.” Itakuwa ni neema ya ajabu, vema, nitakapofika Kule. Kwa hiyo, ninashukuru sana kwa ajili ya baraka Zake.

¹⁶ Ninataka kuwaelekeza, asubuhi ya leo, kwenye Yeremia mlango wa 8, kifungu cha 22.

*Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu?
mbona basi haijapona afya ya binti ya watu wangu?*

¹⁷ Hilo ni fungu dogo sana, bali si jinsi lilivyo dogo, ni thamani iliyo ndani yake. Watu wengi hufuata wingi, bali ni ubora tunaozungumzia.

¹⁸ Hapa wakati fulani uliopita kulikuwako na mvulana mdogo ambaye nilikuwa nikiwaambieni habari zake, aliyepata hiyo juu darini, ng’ambo ya mto kutoka mahali ninapoishi, alipata stempu kuukuu ya posta, iliyoonekana ya manjano. Naye alikuwa na wazo la aiskrimu akilini mwake, kwa hiyo huyo anashuka mtaani kwenda kumtafuta mkusanya stempu, naye akamwuliza, “Utanipa nini kwa stempu hii?”

“Loo,” akasema, “Nitakupa dola moja.”

¹⁹ Mbona, alidhani angepata tu nikeli moja, kwa hiyo akaiuza kwa dola moja. Baadaye kidogo mkusanya stempu huyo akaiuza stempu iyo hiyo kwa dola mia tano, baadaye ilifikia maelfu ya dola, nami sijui ina thamani gani sasa.

²⁰ Sasa, haikuwa kwa sababu ya kile kipande kidogo cha karatasi ya manjano, kwa sababu hapakuwa na faida ya kukiokota sakafuni, cha muhimu ni kile kilichokuwa kwenye karatasi hiyo.

²¹ Na hivyo ndivyo hii ilivyo hapa, ni kile kilicho kwenye karatasi. Biblia hii ilinunuliwa na Ndugu Kidson. Nanii yake. . . Ndugu Kidson alinipa Biblia hii yapata miaka kumi na minne iliyopita huko Houston, Texas, ambako nilikuwa nimefanya mmoja wa miamsho yangu ya kwanza, nami nimehubiri kutokana nayo tangu wakati huo. Biblia hii labda iligharimu

yapata dola ishirini, lakini hayo Maneno niliyosoma hapo ndani ni Uzima wa Milele kwa kila aminiye, ni—ni Neno la Mungu.

²² Ninataka tu kuchukua neno mo—moja kwa ajili ya somo: *Kwa Nini? Kwa Nini?* [Kiingereza: Why?—Mfa.]

²³ Mnajua, kama Mungu akifanya njia ya kuepukia kwa ajili ya watu Wake, nao hawaikubali, basi Yeye anataka kujua ni kwa nini. Kwa nini wakafanya hivyo? Kwa nini...? Nasi, kila mmoja, tutatoa hesabu kwa ajili yake. Mungu anapofanya njia ya uponyaji na watu hawaikubali, basi Yeye anauliza, “Kwa nini?” Anayo haki ya kuuliza ni kwa nini kama hatukubali kile alichotupa.

²⁴ Wakati mmoja katika Biblia, kulikuwa na mfalme, naye alikuwa mfalme wa Israeli. Naye alikuwa ni mwana wa Ahabu na Yezebeli. Basi siku moja alipokuwa akitembea kwenye dirisha la kibaraza chake, a—aliangukia hapo barazani akaumia, akawa mgonjwa sana. Na ndipo akawaita watu wake wawili na kuwatuma huko Ekroni wapate kujua kutoka kwa mungu, Baal-zebubu, mungu mkuu wa nchi hiyo, kama, kumtaka shauri, kama ataishi ama atakufa.

²⁵ Na huko chini kabisa mahali fulani ukingoni mwa kijito, katika kibanda kidogo cha udongo, alikuwako nabii Eliya. Ndipo Mungu akanena na Eliya, naye akaenda akasimama barabarani, na akawasimamisha hawa wajumbe wawili, naye akasema, “Rudini mkamwambie mfalme: ‘Kwa nini atume watu hapa juu kwa mungu huyu? Kwa nini atume watu kwa mungu huyu hapa juu, mungu wa kigeni? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Je, ni kwa sababu hakuna nabii katika Israeli ambaye angeweza kumtaka shauri kuhusu mambo haya? Kwa nini basi, atume watu huko juu?’”

²⁶ Nashangaa leo, wakati mwingine katika makanisa yetu, wakati sisi...kama kuingia hapa asubuhi ya leo...Kwa nini mtu atake kwenda kwenye baa? Kwa nini kijana mwanamke atake kuwa kwenye uwanja wa dansi? Kwa nini watu watake kunywa wiski, kujaribu kutuliza mioyo yao iliyo na huzuni, wakati baraka hizi zote na nguvu za Mungu ziko hapa kwa ajili yetu? Kwa nini tutake ku—kujiandikisha tujipoteze kwenye kanuni fulani za imani ya kimadhehebu, wakati nguvu za Roho Mtakatifu zikiwa hapa kutufanya tuwe na furaha na huru? Kwa nini tutake kufanya hivyo?

²⁷ Inanikumbusha juu ya mtu akifia kwenye vipandio vya mlango wa daktari akiwa na ugonjwa ambao daktari ana tiba yake. Sasa, kama—kama daktari anayo tiba, na mtu huyo ana ugonjwa huo, naye mtu huyo aje barazani mwa daktari, na kwa sababu anafia barazani, akikataa tiba ya daktari, kwa nini, hakuna udhuru, bila shaka hakuna.

²⁸ Kama—kama daktari ana tiba ya ugonjwa alio nao, naye ana chanjo nyingi sana ya, dawa ya kumchanja mtu huyo kutokana

na ugonjwa huo, naye mtu huyo afie kwenye vipandio vya mlango wa daktari, si kosa la daktari, wala si kosa la hiyo dawa, ni kwa sababu mtu huyo hatakunywa hiyo dawa. Hiyo ni kweli kabisa. Ndiyo sababu ya yeye kufa, kwa sababu anakataa kunywa hiyo dawa, hiyo ndiyo sababu anakufa.

²⁹ Na hiyo ndiyo sababu siku hizi, kwamba watu wanafia katika marefu ya kanisa ya dhambi, ni kwa sababu wanakataa kunywa Dawa ambayo Mungu ametoa kwa ajili ya ti—tiba yao ya huzuni zao, ya magonjwa na maradhi, magonjwa ya moyo, nafsi, na akili, watu wanakataa tu kufanya hivyo. Wanasema, “Loo, hilo ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Hilo ni kundi la Wapentekoste.” Nao wanaendelea na kujaribu kunyamazisha kitu hicho kilichobarikiwa ambacho Mungu aliwapa.

³⁰ Hivi uliwahi kuwazia, “Kwa nini mtu hunywa pombe? Kwa nini mtu...? Kwa nini wanawake, wasichana wadogo, wanatoka nje na—na kuonekana kama sherehe ya Mardi Gras, na kuingia kwenye hizi baa duni, na kadhalika?” Ni kwa sababu kuna mahali moyoni mwao panapoonea kiu kitu fulani, naye Mungu aliwamba wapate kuona kiu, ila kumwonea Yeye kiu, nao wanajaribu kutuliza hiyo kiu takatifu iliyobarikiwa kwa mambo ya ulimwengu. Mbona, mnapotosha kitu kile kile ambacho Mungu aliwapa watu kumwonea Yeye kiu. Mnajaribu kuiridhisha kwa mambo ya ulimwengu, haitafanya kazi, kamwe haitafanya kazi.

³¹ Na halafu kama ibilisi hawezi kukufanya ufanye hivyo, anakufanya uende tu uandikishe jina lako kwenye kitabu cha kanisa na kujiita Mkristo, yeye hujaribu kuiridhisha kwa hilo. Lakini hakuna utoshelevu mpaka Mungu Mwenyewe aingie moyoni kudhibiti, na kuwaridhisha watu, na kuwabariki, na kuwapa vitu alivyoviumba moyoni mwao. Anataka kujaza nafasi hiyo, hakuna kitu kingine ulimwenguni kitakachoijsa hiyo. Nyinyi nyote msisahau hilo kamwe.

³² Wasichana, wasichana hawa wadogo hapa, maskini warembo, mliletwa huku mpate kuwa na nywele ndefu, mvae vizuri, bali mtakuwa shabaha ya Shetani. Dumisheni nguvu za Mungu juu yenu wakati wote, msiache ziondoke kamwe, kito hiki kikuu, cha thamani ambapo Mungu ameingia moyoni mwenu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, akitoa hii furaha na shangwe.

³³ Nilipokuwa mvulana, mtoto, nilijaribu kila kitu nilichokuwa mkubwa kutosha kufanya, na mambo mengi ambayo sikuwa mkubwa kutosha kufanya, nilijaribu, kwa vyovyote vile, bali sikupata chochote kilichoridhisha, mpaka Mungu aliponijaza na Roho Mtakatifu, ndipo hilo likaweka kitu fulani moyoni mwangu ambacho kilinipa utoshelevu mkamilifu. Naam.

³⁴ Mnajua jinsi wa—wanavyoifanyia kazi da—dawa kwa ajili ya ugonjwa fulani? Sasa nabii aliuliza, “Je, hapana zeri,” ambayo ni

dawa, “hivi hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Hakuna tabibu ama hakuna dawa? Basi mbona haijarejea afya ya—ya—ya binti ya watu wangu? Kuna shida gani nayo? Husababishwa na nini? Hakuna udhuru.”

³⁵ Sasa, wanapataje dawa? Jambo la kwanza wanalofanya, sayansi hutumia kemikali fulani za a—aina mbalimbali, nao wanaichanganya pamoja katika maabara, na kuweka vijidudu chini ya uchunguzi na kuvimwagia dawa hii, kisha wachukue kijidudu kizuri na kijidudu kibaya, na kufanya kazi pamoja mpaka waweze kupata kitu kitakachokiua hicho kijidudu kibaya, na, isipokuwa iwe ni antibaotiki, na—na kuacha kijidudu kizuri.

³⁶ Sasa, wanapowazia wameikamilisha, wanachukua chanjo hiyo, na kumdunga nungubandia, wapate kuona kama nungubandia huyo ataishi ama atakufa. Sasa, wakati mwingine haitafanya kazi kwa wanadamu. Wala huwezi kuwa na hakika kuhusu dawa, kwa sababu wakati mwingine dawa itakayomsaidia mmoja itamwua huyo mwingine. Nao wanashughulikia namna fulani ya dawa, ama kitu fulani, ku—kujaribu kuponya hiyo kansa.

³⁷ Hivi majuzi, wakati yule mkomunisti alipoinuka na ile chupa, akaitikisa mbele ya ulimwengu, na kusema, “Tuna kitu hapa kitakachomchukua mtu aliyepooza, akiisha kupooza, hali ya misuli imeacha kutenda kazi, na kuirejesha misuli hiyo,” hiyo ni aibu kwa Kanisa. Ukombozi haukutolewa kwa ukomunisti, ukombozi ulitolewa kwa Kanisa, hiyo ni kweli, Kanisa la Mungu aliye hai.

³⁸ Nami nawaambia, badala ya kupekua kurudi kwenye wazo hilo, kanisa linapaswa kuwa likisonga mbele katika nguvu za Mungu, tukichukua mamlaka haya yote makuu tuliyo nayo miongoni mwetu, na si...Sisi...Ninapenda kupiga filimbi, kuna, na—napenda tu, bado kuna utoto kiasi hicho kwangu, napenda kusikia filimbi ikipigwa, lakini hata hivyo, kuweka mvuke mwingi mle ndani kuifanya injini iendeshwe pia, mwajua, inaposhuka kwenye reli. Laiti tungaliweza kupata mahali zilipo nguvu hizi kuu ambazo Mungu ametupa, zitaponya magonjwa, zitatabua mawazo ya moyo, zitawafufua wafu, zitafanya mambo makuu na yenye nguvu kama tu tutaliweka sawa.

³⁹ Sasa, wanasema mwuaji namba moja ni ugonjwa wa moyo, ninatofautiana nao: Mwuaji namba moja ni ugonjwa wa dhambi, huo ndio mwuaji wa taifa, ni ugonjwa wa dhambi. *Dhambi* ni kutokuamini. Inaingia kanisani, inawafunga watu kwenye namna fulani ya theolojia ya kujibunia, lundo la kanuni za imani, na muda si muda mwajua, mtu huyo anakuwa asiyeamini, hata hivyo ni wa kidini, bali asiyeamini.

⁴⁰ Dini ni kitu cha ajabu kufanya kazi nacho, kwa sababu mpinga-Kristo anafanana sana na kitu kilicho halisi, mpaka

itawapumbaza walio Wateule kama yamkini. Kaini alitoa dhabihu kama tu vile Habili alivyotoa, akajenga madhabahu, akainama, akaabudu, akaweka matoleo yake madhabahuni, alifanya kila kitu cha kidini tu kama Habili alivyofanya, bali alikuja kwa njia mbaya, Mungu asingeweza kuipokea.

⁴¹ Naye Yesu alisema, “Wananiabudu bure, wakifundisha Mafundisho, yaliyo maagizo ya wanadamu.” Hatuna budi kupata njia sahihi. Ninasema hivi, ya kwamba mwanadamu kamwe hataweza kumjia Mungu mpaka tutakapoingia kwenye njia imara ya Mungu inayoelekeza mahali hapo.

⁴² Hatuna budi kuua ugonjwa sahihi. Hatuna budi kupata ugonjwa sahihi, na ugonjwa unaopaswa kuuawa ni ugonjwa wa dhambi, kutokuamini. Wala kamwe hatutaupata mpaka tutakapopata Dawa sahihi. Hatuna budi kupata Dawa sahihi, nayo hiyo Dawa sahihi iko katika uchumi wa Mungu mahali fulani, la sivyo Yeye kamwe asingeandika hayo maagizo. Hiyo ni kweli. Kamwe haitafanikiwa mpaka tutakapofika mahali hapo, kufika mahali hapo. Hebu tuichunguze tuone mahali ilipo, tuone kama kuna maagizo, tuone hiyo Dawa ni nini, basi tutakapopata hiyo, basi tumempata huyo mwuaji.

⁴³ Sasa, watu wengine husema, “Vema sasa, ngoja kidogo tu, wajua, siwezi kujizuia kuvuta sigara. Mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa, bali kamwe siwezi kujizuia. Ni—ninaenda kwenye madansi nami si—siwezi kujizuia.”

⁴⁴ Mnajua kuna nini? Hawajakunywa hiyo Dawa bado. Hawajachanjwa, kwa sababu Dawa hii haikujaribiwa kwa nungubandia, Mungu kamwe hakumdunga nungubandia, alijidunga Mwenyewe, kisha akaijaribu mwilini Mwake aone kama ingefanya kazi.

⁴⁵ Sasa, kulikuwako na wakati ambapo hiyo dawa haikuwa nzuri sana, kwa sababu ilidungwa kondoo, na mbuzi, na ndama, na kadhalika, lakini sasa imethibitishwa katika Mungu Mwenyewe, Yeye Ndiye aliyekuja kuinywa hiyo Dawa.

⁴⁶ Ukingoni mwa Yordani, Yeye alichanjwa wakati Mbingu zilipofunguka na Roho wa Mungu akashuka kuja kukaa ndani Yake, alichanjwa, akatembea kwenye kingo za Yordani. Alitoa pepo; wakamtemea mate usoni, Naye akageuza shavu hilo lingine; wakang’oa makonzi ya ndevu, iliwekwa chini ya kila jaribio ambalo ingeweza kuwekwa chini yake, nayo ikathibitika kwamba ni ya kweli.

⁴⁷ Kamwe hakumwomba nungubandia adungwe, alijidunga Mwenyewe, ilikuwa ni kazi iliyohitaji mtu mkubwa. Kwa hiyo, Mungu alifanyika mwili akakaa kwetu apate kudungwa hiyo Dawa. Yeye Ndiye aliyeigundua, Yeye Ndiye aliyejaribu Mwenyewe, hakumwomba mtu mwingine yeyote kuinywa, aliinywa Mwenyewe mwilini Mwake Mwenyewe.

⁴⁸ Ndipo tunaona, kwenye ile siku msalabani alipokuja kukabiliana na mauti, hiyo Dawa ilishikilia, hiyo Sumu ilikuwa ni ya kweli, ilikuwa sahihi. Waligundua wakati walipomtemea mate, Yeye angali angeweza kuwaombea, walipopigilia misumari mikononi Mwake, Yeye alisema, “Wasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.” Yeye—Yeye alitenda yale aliyohubiri, alitenda vivyo hivyo hasa, kwa sababu ile Dawa aliyochanjwa nayo, ilishikilia.

⁴⁹ Mtu aliuliza wakati mmoja, “Mwanangu anaweza kuketi mkono wa kulia na wa kushoto?”

⁵⁰ Akasema, “Hiyo si yangu kutoa, lakini je, unaweza kudungwa Chanjo ile ile ambayo nimechanjwa? Je, unaweza kudungwa Chanjo ya Mungu?”

⁵¹ Halafu pale Kalvari, ilithibitika kwamba ilistahimili, ilikuwa sawa. Sasa, thibitisho linakuja, je, itawafufua wafu? Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka ile Chanjo ingali ilistahimili, kwa kuwa ile mihuri ilivunjwa kaburini, Malaika wa Bwana alishuka, nalo lile jiwe likaondolewa, naye Mwana wa Mungu aliyekuwa kaburini, Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili miongoni mwetu, alitoka akaja kuthibitisha ya kwamba hiyo Chanjo ingestahimili katika majaribu, katika ugonjwa, katika mauti, na katika ufufuo, ingali ingestahimili.

⁵² “Kwa nini binti ya watu wangu ni mgonjwa? Je, hapana zeri katika Gileadi?” Kuna nyingi sana, Yeye aliimwaga kutoka Juu. Wakati wanafunzi walipoona, pamoja na watu waliokusudiwa Uzima wa Milele walipoona ile Chanjo ambayo ingeweza kugeuza shavu upande *ule* na upande *ule*, Ile ambayo ingeweza kukabiliana na mauti na kuwa na hakikisho ya kwamba Maandiko yalikuwa sahihi . . .

⁵³ Mtu anapochanjwa Chanjo ya Mungu, ambayo ni Roho Mtakatifu, atakubaliana na kila Neno ambalo Mungu alisema. Kamwe hawataikatakata Biblia kwa kisu kuchukua baadhi ya theolojia ya watu fulani, atachukua kila Neno ambalo Mungu aliandika, litasema, “Ni kweli. Ni kweli.”

⁵⁴ Yesu alikuwa na ukweli, kwa sababu Mungu alisema kupitia kwa nabii, “Sitamwacha Mtakatifu wangu aone uharibifu, wala sitaiacha Nafsi Yake katika kuzimu.” Hiyo ilikuwa ndiyo sindano iliyopenya kwenye mishipa Yake, bali kwenye asubuhi ya Pasaka Yeye alijua ya kwamba angetoka humo, kwa sababu Biblia ilikuwa imesema hivyo. Nao uharibifu unaingia katika saa sabini na mbili, siku tatu mchana na usiku ingemlazimu kufufuka la sivyo Maandiko yangevunjwa. Kwa hiyo, Maandiko hayawezi kuvunjwa, hayawezi kuvunjwa, Mungu aliliahidi hilo, liishieni tu kikamilifu.

⁵⁵ Kulikuwa na watu mia na ishirini waliotaka Chanjo ile ile siku moja. Walikuwa wamemwona. Loo, Mungu asifiwe! Yesu alisema, “Kama mkitaka Chanjo, nendeni kule Yerusalemu

mkangoje. Msisisimkwe, ngojeni tu, nitaituma. Tuna maagizo yake yote huko juu.”

⁵⁶ Nao walikuwa wakingojea, na mara ikaja sauti kutoka Mbinguni, ile Chanjo ilikuwa njiani Mwake, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, nayo ikajaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia, kama moto, wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na kuanza kunena kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka.

⁵⁷ Shida ilikuwa ni nini? Walikuwa wamedungwa chanjo. Loo, walipotoka nje mtaani, basi wakaanza kuona udhihirisho wa Mungu, ndipo watu wakaanza kulia, wakisema, “Vema, mambo haya yanamaanisha nini? Haya yote yanahusu nini? Nasi tufanye nini tupate kuokolewa?”

⁵⁸ Sasa, Mungu akaweka mhu-...si mhubiri, bali daktari katika Kanisa Lake. “Je, hakuna tabibu? Hivi hapana chanjo? Hivi hapana zeri? Hivi hapana...?” Pana zeri nyingi sana, walikuwa wameiona. Sasa, wana daktari atakayeandika maagizo sahihi. Naam, bwana! Daktari Simoni Petro aliwaambia la kufanya, alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtampokea Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

⁵⁹ Petro kamwe hakusema, “Haya ni maagizo tu ya leo.” Ni maagizo kwa watoto wenu, na kwa watoto wa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Maagizo hayo yalifanya kazi kwao, maagizo hayo yalifanya kazi juu yangu, maagizo hayo yatafanya kazi kwako, ambayo, maagizo, yatafanya kazi kwa kila mtu ambaye Bwana Mungu anamwita.

⁶⁰ Sasa, ulimwengu una shida gani? Ni mgonjwa kwa dhambi. Haya hapa maagizo yameandikwa, kuna Dawa nyingi sana. Niliihisi asubuhi nzima, ingali iko mwilini mwangu mwote sasa, nami ninajua ya kwamba Dawa hiyo ina Uzima wa Milele ndani Yake, kwa kuwa iliniinua kutoka maskini mwenye dhambi kunifanya Mkristo, mwaminio wa Mungu. Kitu fulani kiliichochea nafsi yangu na kunituma kote ulimwenguni, Tommy Osborn, watu mbalimbali, kitawatuma.

⁶¹ Kanisa lina shida gani? Ni kwa sababu wanakataa kuchukua maelekezo ya dawa, hakuna lingine. “Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?” Loo, naam, tuna madaktari, tuna zeri. Mbona, hatutawapa maagizo ya uongo, tutawaandikia kitu sahihi, hasa kabisa.

⁶² Petro alisema, “Haya ndiyo maagizo.” Dk. Simoni Petro alikuwa na wazo sahihi.

⁶³ Akasema, “Tufanye nini? Itadumu muda gani?”

64 Yeye akasema, “Kwenu ninyi, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Maagizo haya yatafanya kazi, yatawachanja watu kutoka dhambini, kama tu watachukua maagizo hayo.

65 “Tufanye nini tupate kuokolewa?”

66 Ndipo akaandika hayo maagizo. “Pana zeri katika Gileadi, pana Dawa, na pana madaktari pia.”

67 Basi kwa nini watu wanakufa? Kwa nini watu wanakufa katika dhambi zao? Kwa sababu wanakataa kuchukua maelekezo ya dawa na kuyatekeleza. Mnaamini hilo?

68 Roho Mtakatifu yupo hapa sasa, Hii ni—Hii ndiyo Dawa ya Mungu kwa kila nafsi iliyo na ugonjwa wa dhambi, Dawa ya Mungu, Roho Mtakatifu. Loo, na—najisikia kana kwamba haikuwa imechelewa sana, ninaamini ningeweza kuhubiri sasa hivi, kwa namna fulani ninajichangamsha, ninajisikia vizuri tu.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

69 Bwana Yesu, Mpaji mkuu wa Uzima wa Milele, Baba mkuu wa Roho wa wenye haki, tunakushukuru, Ee Bwana, kwa ajili ya wema Wako na kwa rehema Zako. Ninataka kukushukuru Wewe Bwana, kwa ajili ya kanisa hili dogo, kwa yote linayotetea, na wema wake, na ninii yake... na mambo ambayo limefanya katika Jina Lako.

70 Ee Baba Mungu, Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, na Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, ndani Yake, nao wanakuwa salama. Loo, katika nchi hii yenye uchovu, ambako tumesafiri na kuona watu wamemezwa ulimwenguni, makanisa ya kawaida, yasiyojali, yakifa katika dhambi, kwa sababu yanaikataa Dawa, ni jambo la ajabu jinsi gani kuingia katika Uwepo wa Mwamba huo katika nchi yenye uchovu! Loo, kanisa hili na lisimame hivyo daima, Baba. Jalia lisimame, limejaa Dawa. Ee Bwana Mungu, tujalie. Jalia watu waliochoka waingie hapa na kuokolewa. Tujalie, Bwana. Wape... .

71 Mbariki Ndugu yetu Williams, wote wawili, Mkubwa na Mdogo. Mbariki mmishenari huyu anayeingia hudumani, wachungaji wanaoshirikiana, na watu mbalimbali kutoka makanisa mbalimbali. Ndugu yetu mpendwa sana Tommy Osborn, Bwana, uwe pamoja naye anaposafiri mahali mahali kote ulimwenguni, mpe watu.

72 Liweke kanisa hili dogo, kama ilivyoandikwa, “mahali pa kujificha wakati wa dhoruba,” ili tuweze kuingia mbio, na, kutoka kwenye huduma za umishenari, na kuzitia moto nafsi zetu, tupate viburudisho, Ee Bwana, kuketi chini kwenye kivuli cha Mwamba na kumsikia Malaika wa Bwana akizungumza nasi. Jinsi tunavyoshukuru kwa ajili yake! Omba ya kwamba kamwe hazitaninii, jalia hizi taa zisififie kamwe, jalia hilo

pipa lisipunguke wala hii chupa isiishe, Bwana. Jalia watoto wa Mungu walishwe kutoka kwa madaktari halisi, ambao wataandika maelekezo dhahiri na safi ya dawa, na kuhubiri Neno pasipo kupatana juu ya lolote la Hilo.

⁷³ Jalia uamsho wa Roho Mtakatifu uje kupitia hapa, Baba, kama vile ndugu alivyosema muda mfupi uliopita, jalia uwake moto ndani ya kila moyo mpaka watu walio wagonjwa wa dhambi waweze kuchanjwa kutokana na dhambi, ili waweze kuwa na ujasiri, na matumaini ya kufufuka kwa Bwana Yesu kukiwajia katika siku za mwisho. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

⁷⁴ Ni wakati mzuri sana! Loo, hii ni kama Mbinguni kwangu.

⁷⁵ Mtu yeyote aliye mgonjwa, inua mkono wako, useme, “Ninataka kuombewa.” Mungu ndiye Mponyaji. Mungu ni Mponyaji mkuu.

⁷⁶ Kwa dakika arobaini na tano zilizopita, kumekuwa na jina limeendelea kuja mbele yangu, sijui ni kwa nini. Labda itakuwa mkutanoni, ama mahali fulani, sijui. Jina ni... Ni mtu fulani anayeomba, ama mtu fulani anayejiandaa kutaka kitu fulani, sijui ni kitu gani, lakini chochote kile, Bwana atakijalia. Jina hilo linaonekana kama linasema, Kozard, ama kitu fulani, K-o-z-a-r-d ama kitu kama hicho. Inaonekana tu kana kwamba ninaendelea kuliona, ama kitu fulani kinacholia masikioni mwangu cha “Kozard, Kozard,” ama kitu kama hicho, K-o-z-a-r-d. Labda mtu fulani angekuwa mkutanoni, mahali fulani, kwamba li—litatukia, lakini linaendelea tu kulia moyoni mwangu, na mbele yangu ninaendelea kuona jina hilo. Mtu fulani akiomba kitu fulani, mahali fulani.

⁷⁷ Sasa, Bwana Yesu anajua mambo yote, Yeye—Yeye hutoa na kujiandaa kwa ajili ya kila kitu. Sasa, kama wewe ni mgonjwa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

⁷⁸ Ee Bwana... 

60-0401M Kwa Nini?
First Apostolic Church
Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org